# Saratani ya Ini



American Liver Foundation
www.liverfoundation.org
**1-800-GO-LIVER**

AMERICAN LIVER FOUNDATION
*Your Liver. Your Life.*

## Ni kwanini ini ni muhimu?

Ini ni ogani ya pili kubwa zaidi katika mwili wako na inapatikana chini ya kizimba cha mbavu kwenye upande wa kulia. Ina uzani wa kama pauni tatu na umbo lake ni kama mpira wa soka ambao umelala upande mmoja.

Ini hufanya kazi nyingi katika mwili wako. Huwa inachakata kile unachokula na kunywa kuwa nguvu na virutubishi ambavyo mwili wako unaweza kutumia. Ini pia hutoa vitu vyinavyoweza kukudhuru kutoka kwa damu yako.

## Saratani ya ini ni nini?

Saratani ya ini ni kukua na usambazaji wa seli zisizo na afya kwenye ini. Saratani ambayo huanza kwenye ini ni saratani ya kimsingi ya ini. Saratani ambayo inasambaa kwa ini kutoka kwa ogani nyingine ni saratani enezi ya ini.

Karibu Waamerika 21,000 wanapatikana na saratani ya kimsingi ya ini kila mwaka. Saratani ya kimsingi ya ini ni moja ya saratani chache zinazoongezeka huko Amerika. Saratani ya kimsingi ni kama mara mbili zaidi kwa wanaume kuliko wanawake.

## Saratani ya ini inasababishwa na nini?

Kuna hatari kadhaa za saratani ya ini.

- Cirrhosis (vidonda kwenye ini) inaweza kusababisha saratani ya ini. Huko Amerika, unywaji pombe kupindukia na Homa ya Virusi ndio chanzo kubwa za cirrhosis.
- Uambukizaji wa muda mrefu wa Homa ya Maini na Homa ya Virusi unahusishwa na saratani ya ini kwa sababu mara nyingi husababisha ugonjwa wa cirrhosis. Homa ya Maini inaweza kusababisha saratani ya ini bila cirrhosis.
- Ugonjwa wa kunona sana huongeza hatari ya kupata saratani ya ini.
- Ugonjwa wa sukari unaweza kuongeza hatari ya saratani ya ini, haswa kwa wale ambao hunywa pombe sana au wanayo virusi vingi vya hepatisis.

## Dalili za saratani ya ini ni nini?

Mara nyingi hakuna dalili za saratani ya ini hadi ugonjwa uwe katika kiwango cha juu zaidi. Wakati dalili zinatokea, zinaweza kuwa pamoja na, kufura tumbo, uchungu katika upande wa tumbo ya juu au mgongo na mabega, kichefuchefu, kupoteza hamu ya chakula, hisia za kushiba, upotezaji wa uzani, udhaifu, homa ya nyongo ya manjano (macho na ngozi kuwa manjano).

## Je! saratani ya ini inagunduliwa vipi?

Saratani ya ini inagunduliwa kwa uchunguzi wa kimwili au kwa uchunguzi wa picha. Ili kudhibitisha uchunguzi wa saratani ya ini, madaktari hutumia upimaji damu, vipimo vya maabara, uchunguzi wa tomografia ya kompyuta (CT), uchunguzi wa picha za sumaku (MRI), na andiogramu. Daktari wako pia anaweza kuhitaji uchunguzi wa giligili na tishu za kusababisha ugonjwa (biopsy). Wakati wa kuchunguza giligili, kipande kidogo cha tishu ya ini hutolewa na kuchunguzwa katika maabara.

## Saratani ya ini inatibiwa vipi?

Matibabu ya saratani ya ini hutegemea:

- hali ya ini
- Ukubwa, sehemu, na idadi ya uvimbe
- Ikiwa saratani imesambaa nje ya ini
- umri wa mtu na afya kwa jumla

Chaguo za matibabu ikiwa saratani haijasambaa na sehemu nyingine yote ya ini iko sawa ni:

**Pandikiza**
Ikiwa saratani haijasambaa, kwa wagonjwa wengine pandikizo la ini (ubadilishi ini) inaweza kuwa chaguo.

**Upasuaji**
Ikiwa saratani imepatikana katika hatua yake ya mapema na sehemu nyingine ya ini iko sawa, madaktari wanaweza kufanya upasuaji ili kutoa uvimbe kutoka kwa ini (upasuaji wa sehemu ya ini).

Chaguo zingine za matibabu ikiwa upasuaji na pandikiza haziwezekani ni pamoja na:

**Utumiaji wa giligili baridi zaidi za nitrojeni kuua tishu ambazo hazitakikani**
Hutumia kipima kidonda cha chuma kugandisha na kuua seli za saratani.

**Upasuaji wa sehemu au tishu za saratani kutumia nguvu za elektromagnetiki**
Hutumia kipima kidonda maalum kuua seli za saratani kutumia moto.

**Sindano ya Ethanoli**
Pombe ya Ethanoli hudungwa ndani ya uvimbe wa ini ili kuua seli za saratani.

**Tibakemikali au tibakimo**
Tibakemilaki hutumia dawa kuua seli za saratani. Katika hali zingine, tibakemikali inaweza kudungwa moja kwa moja ndani ya uvimbe wa ini.

**Matibabu ya kutumia Mnururisho**
Matibabu ya kutumia mnururisho hutumia mnururisho (wa nishati ya juu Eksirei) ili kuua seli za saratani.

**Sorafenib (Nexavar)**
Sorafenib ni dawa ya kunywa ya FDA iliyoidhinishwa kutumiwa katika hali kali ya hepatocelluar carcinoma (aina inayojulikana zaidi ya saratani ya kimsingi ya ini).

## Je! ni njia gani bora za kuzuia hatari ya saratani ya ini?

Hatua za kupunguza hatari ya saratani ya ini ni pamoja na:

- Kuona daktari mara kwa mara ambaye ni mtaalam wa saratani ya ini.
- Zungumza na daktari wako juu ya uzuiaji wa virusi vya hepatisis,pamoja na chanjo za hepatisis A na Homa ya Maini.
- Chukua hatua ili kuzuia uwazi wa kupata Homa ya Maini na Homa ya Virusi.
- Ikiwa unayo cirrhosis au ugonjwa kali wa ini, fuata mapendekezo ya daktari wako ya matibabu na kuwa unachunguzwa kila mara kwa saratani ya  ini.

- Ikiwa una uzani mzito au ugonjwa wa kunona sana, ugonjwa wa sukari au unakunywa pombe zaidi, zungumza na daktari wako juu ya afya ya ini na uchunguzi wa saratani ya ini.

## Kweli katika Mtazamo wa Haraka

- Saratani ya ini ni kukua na usambazaji wa seli zisizo na afya kwenye ini.
- Saratani ambayo huanza kwenye ini ni saratani ya msingi ya ini. Saratani ambayo inasambaa kutoka kwa ogani nyingine ni saratani enezi ya ini.
- Karibu Waamerika 21,000 wanapatikana na saratani ya kimsingi ya ini kila mwaka.
- Saratani ya kimsingi ya ini ni mojawapo ya saratani chache zinazoongezeka huko Amerika.
- Saratani ya kimsingi ni kama mara mbili zaidi kwa wanaume kuliko wanawake.
- Mambo hatari ya saratani ya ini ni magonjwa mengine ya ini (haswa cirrhosis, Homa ya Maini kali na Homa ya Virusi kali).
- Mara nyingi hakuna dalili za saratani ya ini.
- Madaktari mara nyingi hupendekeza uchunguzi wa mara kwa mara wa saratani ya ini kwa hatari kubwa ya saratani ya ini.
- Saratani ya ini inagunduliwa kwa uchunguzi wa kimwili au kwa uchunguzi wa picha.
- Matibabu yanategemea hali ya ini, ukubwa, sehemu, na idadi ya uvimbe, ikiwa saratani imesambaa nje ya ini, umri wa mtu na afya kwa jumla.

American Liver Foundation
www.liverfoundation.org

**1-800-GO-LIVER**

Uchapishaji wa brosha hii umewezeshwa na ruzuku ya ufidhili kutoka kwa huduma ya Afya ya Bayer Pharmaceuticals na Onyx Pharmaceuticals.

©2009 American Liver Foundation. All rights reserved.